

ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba”(Wafilipi 2:5-8).

Mambo yanayoongelewa hapa juu ya Yesu ni ukweli ambao hakuna mtu yeyote aliyewahi kuishi kuitwa hivi. Kama vile yule akida alivyotamka, akiwa amesimama mbele ya msalaba wa Kristo akimwangalia Mwana wa Mungu aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, *“Hakika huyu alikuwa mwana wa Mungu”* (Mathayo 27:54). Yeye ni Mwana wa Mungu! Na wala sio mwanadamu tu. Yeye si miongoni mwa malaika! Ni zaidi ya malaika! Yeye ndiye Mwana pekee wa Mungu!

Waraka mzima kwa Waebrania unaonyesha tofauti kati ya Sheria za kale za Musa na Agano Jipya la Kristo. Pia kinamwinua Yesu juu ya yote. Waraka huu unaanza, *“Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu. Yeye kwa kuwa ni mng’ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake, akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake, akiisha kufanya utakaso wa dhambi, aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko juu; amefanyika bora*

kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao” (Waebrania 1:1-4).

Ni wazi kwamba Yesu Kristo ni zaidi ya vyote, na ya kuwa, hata sasa yuko mkono wa kuume wa Mungu, akiwa Kuhani wetu Mkuu, akiwa Mfalme katika ufalme wake wa kiroho, yaani kanisa. Pia, ni wazi kwamba kwa njia ya utii wa injili yake, tunaweza kufanyika kuwa raia wa ufalme wake wa kiroho, mwili wake ambaye yeye ndiye kichwa. Hivyo, kwa kudumu kuishi kwa uaminifu katika mwili wake, siku moja tunaweza kuishi milele pamoja naye. Ili kuwa kiungo katika kanisa lake, mwili wa waliookoka, lazima tumwende Mungu kupitia Yesu, tukimwamini Kristo kuwa Mwana pekee wa Mungu (Yohana 8:24). Kisha tunapaswa kutubu dhambi zetu; yaani, kubadilisha nia zetu na kisha maisha yetu, tukigeuka na kuwa mbali na dhambi (Luka 13:3). Tena ni lazima tumkiri Yesu kuwa ndiye Kristo, Mwana wa Mungu na kuzikwa katika ubatizo ili tupate msamaha wa dhambi zetu (Matendo 8:36-39). Ndiposa tunakuwa tumesafishwa kwa damu ya Kristo, na kuzidishwa na Bwana katika kanisa la Kristo, ambalo limenunuliwa kwa damu yake ya thamani (Matendo 2:41,47; 20:28).

YESU

NI

NANI?

(Who is Jesus- Kiswahili)

Tuandikie:

International Bible Teaching
Ministries
www.IBTMinistries.org